# OFISI YA RAIS- TAMISEMI

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NGORONGORO

**Shule ya Sekondari L. Natron.**

**S.L.P. 88,**

**<u>LOLIONDO.</u>**

**Tarehe: 01/12/2023**

Kumb. Namba. LN/SS/AD/VOL.1-13

Mzazi/Mlezi wa ………………………………………………….

S/M……………………………………………………………..

S.L.P………………………………………..

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI LAKE NATRON.**

## 1.0. UTANGULIZI.

Ninafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza mwaka 2024 katika shule ya Sekondari Lake Natron .

Shule hii ipo mkoa wa Arusha, Wilaya ya Ngorongoro, Tarafa ya Sale, Kata ya Engaresero, Kijiji cha Engaresero, Kitongoji cha Monik umbali wa kilometa 100 kutoka makao makuu ya wilaya. Namna ya kufika shuleni hapa ni kupitia mabasi kama ifuatavyo; Kutoka Loliondo lipo basi liendalo Arusha kupitia eneo la shule kila siku, kutokea Arusha mjini mabasi hupitia eneo karibu na shule kila siku.

Muhula wa masomo utaanza tarehe 08/01/2024 siku ya jumatatu.

Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 06/01/2024 saa mbili asubuhi mpaka saa kumi jioni na mwisho wa kuripoti ni tarehe 26/01/2024 saa kumi jioni na siyo zaidi ya hapo.

## 2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### A. SARE ZA SHULE

i. Sare za shule hii ni kama ifuatavyo; Suruali pea mbili rangi ya moromboso na mashati mawili meupe ya mikono mifupi

ii. Wasichana sketi mbili ndefu zinazokaribia kufika chini rangi ya moromboso na mashati mawili meupe

iii. Sweta la rangi ya dark bluu kwa wote

iv. Viatu vyeusi vya ngozi visivyo na visigino virefu na vya kamba pea mbili.

v. Soksi pea mbili rangi nyeusi kwa wavulana na wasichana pea mbili nyeupe.

**B. SARE ZA KUFANYIA KAZI (SHAMBA DRESS)**

i. Wavulana suruali mbili za rangi ya kijani (jani la mgomba)
ii. Wasichana sketi mbili za rangi ya kijani (jani la mgomba)
iii. T-shet 2 zenye nembo ya shule zinapatikana shuleni kwa gharama ya @ 12,000/
iv. Kanga au kitenge pea 1 kwa wasichana.

**NB: Kwa atakayeona inafaa fundi wa kushona sare anapatikana mazingira ya karibu na shuleni**

## C. SARE ZA MICHEZO

i. Aje na trucksuit moja yenye mhuri wa shule kwa wote. Hii utaipata shuleni kwa Tsh. 30,000/=
ii. Aje na T-shirt na suruali ya michezo rangi ya njano kwa wote
iii. Aje na raba za michezo (nyeupe kwa wasichana) na kwa wavulana rangi yoyote

**MUHIMU: Mwanafunzi haruhusiwi kuja na nguo za nyumbani hata moja**

## D. VIFAA VYA MASOMO DARASANI

i. Madaftari makubwa 11 (counter books quire 2 au 3)
ii. Kamusi ya kiingereza, (Oxford English – English Dictionary)
iii. Faili moja (Spring file) kwa ajili ya kutunzia mitihani na mazoezi mengine
iv. Kofa moja (Mathematical set)
v. Karatasi za matumizi ya mwanafunzi (Ream 1)
vi. Kalamu, penseli, rula pamoja na daftari tano zenye kurasa 80/90 kwa ajili ya kozi ya Kiingereza kuanzia kidato cha kwanza

## 3.0. MAHITAJI YA MWANAFUNZI BWENINI

i. Godoro lenye upana futi mbili na nusu kwa nchi tatu aina ya Tan foam au Comfy. Kuondoa usumbufu wa kusafirisha magodoro yanapatikana karibu na shuleni kwa Tsh. 40,000/=
ii. Aje na chandarua chenye dawa
iii. Aje na shuka pea mbili kwa wasichana rangi ya pinki, kwa wavulana rangi ya bluu
iv. Aje na vyombo vya kulia chakula yaani sahani, bakuli, kikombe na kijiko na visiwe vya plastiki
v. Aje na fagio ngumu (hard broom) 01, rubber squizer 01 na fagio ya chelewa 01
vi. Taulo kwa ajili ya kuogea
vii. Aje na nguo za ndani kuanzia tano kwa wavulana na kumi kwa wasichana
viii. Aje na mswaki pamoja na dawa kwa ajili ya usafi wa kinywa
ix. Aje na toilet paper tano na kuendelea kwa ajili ya matumizi ya chooni
x. Aje na pedi za kutosha kwa wanafunzi wa kike
xi. Aje na ndoo ndogo moja ya lita kumi kwa ajili ya matumizi yake binafsi
xii. Aje na tochi kwa ajili ya kumulika wakati wa usiku wakati wa kwenda kulala wakitoka darasani
xiii. Sanduku la chuma/bati kwa ajili ya kutunzia vifaa vyake

xiv. Mzazi umpatie mwanao fedha za nauli za kuja nyumbani kipindi cha likizo

xv. Mpatie mwanao fedha za kukata bima ya afya Tsh 6000/ kwa mwaka na fedha za matumizi, huduma ya kwanza inapatikana shuleni.

**NB: Ili kuepuka kubeba mizigo mingi na gharama za usafirishaji, mahitaji yote yaliyotajwa hapo juu yanapatikana maduka yaliyopo karibu na shuleni unaweza kuja kununulia hapa isipokuwa sanduku la chuma.**

**Karibuni sana Lake Natron Sekondari**

**Martin N. Mondeya**
**MKUU WA SHULE (0784630717)**

**Nakala;**

1. **Mkurugenzi Mtendaji,**
   **Halmashauri ya (W) Ngorongoro**
   **S.L.P 01**
   **LOLIONDO.**

2. **Afisa Elimu Sekondari (W),**
   **S.L.P 01,**
   **LOLIONDO.**

3. **M/kiti wa Bodi**
   **Shule ya Sekondari Lake Natron.**

## SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama iliyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu mwanafunzi awapo shuleni anapaswa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara utakaporipoti shuleni.

i. Heshima kwa viongozi, wazazi na wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii nzima kwa ujumla ni jambo la lazima
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
iii. Kushiriki kwa makini kufanya maandalizi ya jioni ( Night preparation)
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine atakazopangiwa
v. Ni marufuku kupigana shuleni, ukipigana utafukuzwa shuleni
vi. Ni marufuku kutukana shuleni
vii. Ni marufuku kupata mimba/ kumpa mimba mwanafunzi mwenzako
viii. Ni marufuku kuvuta sigara, bangi na madawa ya kulevya ukikamatwa utafukuzwa shule
ix. Kutii kengele ni jambo la lazima
x. Lazima kutii bendera ya Taifa na wimbo wa Taifa.

## MEDICAL EXAMINATION FORM

***This form must be completed by government Medical Officer***

Student's full name…………………………………………………………………………………………………

T.B. Test …………………………………………………………………………………………………………

Urine Analysis…………………………………………………………………………………………………

Blood pressure…………………………………………………………………………………………………

Eye Test…………………………………………………………………………………………………………

Ear Test…………………………………………………………………………………………………………..

Widal Test ………………………………………………………………………………………………………

Pregnancy Test…………………………………………………………………………………………………

BS Test……………………………………………………………………………………………………………

H.I.V Test……………………………………………………………………………………………………….

Brucellosis Test………………………………………………………………………………………………….

Additional information; please if there is any case detected apart from the above mentioned, try to inform the school through this form for better future of the child and the school at large.

**TO BE FILLED BY THE GOVERNMENT MEDICAL OFFICER.**

***I certify that the above mentioned student is able? Not able to pursue his/her studies.***

***Signature and rubber stamp………………………………***

***Designation………………………………………***

***Station…………………………………………………***

***Date of ……………………………………………………..***